

# **TANGAZO**

## **KUSIKILIZA KERO ZA WANANCHI MANISPAA YA SONGEA**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya nchini kote kuhakikisha kuwa kero zote za wananchi ambazo zipo ndani ya uwezo wao zinamalizwa haraka.

Ili kutekeleza agizo hilo, Halmashauri ya Manispaa ya Songea imeteua siku ya Alhamis kuwa siku maalum ya kusikiliza kero na migogoro toka kwa wananchi ili Halmashauri iweze kuishughulikia katika ngazi ya Halmashauri.

Lengo la Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni kuhakikisha inatatua haraka iwezekanavyo kero na migogoro yote inayowakabili wananchi.

Tunaomba wananchi wote wenye kero na migogoro mbalimbali wafike ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea siku ya Alhamis kuanzia majira ya saa 4.00 asubuhi.